



TAARIFA ZA YA HARAKA

Vipindi vya Kujiandikisha

Wakati wa cha mwaka ambapo unaweza kujiandikisha katika mpango wa bima ya afya unategemea aina ya mpango wa bima ya afya kwa ambao unastahiki.



Mtandaoni kwenye
nystateofhealth.ny.gov



Kwa nambari ya simu
1-855-355-5777

TTY
1-800-662-1220



Mtembelee Msaidizi wa Ana
kwa Ana

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, jinsia, umri au ulemavu katika mipango na shughuli zake za afya.

Je, mbona ujiandikishe katika mpango wa bima ya afya kupitia NY State of Health?

Kuna sababu nyingi za kujiandikisha katika bima ya afya na NY State of Health inarahisisha kutafuta na kujiandikisha katika bima ya kina na ya gharama ya chini. Kuna mipango mingi ya bima ya afya ya kuchagua. Unaweza kupata usaidizi kutoka kwa msaidizi mwenye mafunzo. Na, unaweza kufuzu kupata bima ya bila malipo au kupata usaidizi wa kulipia bima yako.

Je, NY State of Health inatoa mipango ipi ya bima?

NY State of Health ndipo mahali pa kutafuta na kujiandikisha katika **Medicaid, Child Health Plus, Bima Msingi, na Bima za Afya Unazofuzu.**

Je, ninaweza kujiandikisha lini?

Wakati unapoweza kujiandikisha unategemea ni kwa mpango upi unastahiki jambo linalotegemea umri, pato na vipengele vingine. Uandikishaji uko wazi mwaka mzima ikiwa unastahiki kwa:

- Medicaid
- Child Health Plus
- Bima Msingi

Unaweza kujiandikisha katika **Bima za Afya Unazofuzu** wakati wa Kipindi Wazi cha Uandikishaji cha kila mwaka, au Kipindi Maalum cha Uandikishaji, ikiwa unastahiki.

Wahindi Wamarekani na Wazaliwa wa Alaska wanaweza kujiandikisha wakati wowote mwakani kwa mpango wowote wa NY State of Health.

Je, Kipindi Wazi cha Uandikishaji ni nini?

Kipindi Wazi cha Uandikishaji ni muda mfupi wa mwaka – kwa kawaida Novemba hadi Januari – unapoweza kujiandikisha katika Bima za Afya Unazofuzu. Usipojiandikisha katika miezi hii, utahitaji kusubiri hadi Kipindi Wazi cha Uandikishaji kijacho. Kuna baadhi ya vighairi. Unaweza kujiandikisha katika Bima za Afya Unazofuzu nje ya Kipindi Wazi cha Uandikishaji ikiwa Unastahiki kwa Kipindi Maalum cha Uandikishaji.

Je, Kipindi Maalum cha Uandikishaji ni nini?

Kipindi Maalum cha Uandikishaji ni wakati mtu anapokuwa na tukio maalum maishani (linaloitwa “Tukio Maishani Linalofuzu”) linalomwezesha kujiandikisha katika au kubadilisha bima yake kupitia Bima za Afya Unazofuzu nje ya Kipindi Wazi cha Uandikishaji.

Je, ni Matukio yapi Maishani Yanayofuzu yanayoweza kumfanya mtu kustahiki kwa Kipindi Maalum cha Uandikishaji?

Matukio Maishani Yanayofuzu yanajumuisha:

- Upotezaji bima ya afya (kwa sababu kando na kutolipa ada yako ya bima)
- Kuhamia kabisa Jimbo la New York au kuhamia ndani ya Jimbo ambalo linakupa mipango mipya ya bima ya afya
- Uhusiano wa ndoa au wa kinyumbani (lazima uwe ulikuwa na bima nyingine siku 60 zilizopita)
- Talaka au kutengana kisheria
- Ujauzito uliothibitishwa na mtaalamu wa afya
- Mtoto Kuzaliwa au kutwaaliwa, au mtoto kuwekwa chini ya ulezi wa kambo
- Kuwa unastahiki au haustahiki kwa usaidizi wa kulipia bima yako ya Bima za Afya Unazofuzu
- Kuwa raia au mtu aliyepo kisheria

Kwa jumla, ni lazima uripoti Tukio Maishani Linalofuzu kwa NY State of Health ndani ya siku 60. Huenda ukahitajika kutoa ithibati ya Qualifying Life Event kwa mpango wako mpya wa afya au NY Stat of Health.

Je, nitajua vipi ninastahiki kwa mpango upi?

Kuna njia tatu rahisi za kujua kama unastahiki kwa bima ya afya:

- Tuma ombi mtandaoni kwa nystateofhealth.ny.gov
- Pigia simu Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa nambari **1-855-355-5777**
- Kutana na msaidizi wa ana kwa ana



Mtandaoni kwenye
nystateofhealth.ny.gov



Kwa nambari ya simu
1-855-355-5777

TTY
1-800-662-1220



Mtembelee Msaidizi wa Ana
kwa Ana

Tutakusaidia kwenye mchakato kamili wa uandikishaji, tukujulishe ni kwa mpango upi unastahiki, na wakati unaoweza kujiandikisha. Usaidizi unapatikana kwa lugha yoyote yoyote ile unayozungumza.